


PLEASE RETURN THIS
BOOK.

IWE NURU

Katika njia zako zote

mkiri yeye


...Mithali 3: 6



BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE

P.O. Box 30370,

NAIROBI.



JULY, AUGUST, SEPTEMBER

1967

•
•
(• (

() • (

I W E N U R U

Julai - Agosti - Septemba

1967

Y A L I Y O M O

JULAI - UKRISTO DHAHIRI

Huru Kutoka kwa Sheria!
Tunda la Roho: Upendo, Furaha, Amani
Tabia Mbele ya Binadamu na Mbele ya Mungu
Mawazo Juu ya Wagalatia 5

AGOSTI - TABIA YA MWANAMKE MKRISTO

Mwanamke Anatoa Shauri
Shauri la Mama Juu ya Kunywa na Kuwasaidia Maskini
Vitendo vya Mwanamke Mwema
Wajibu na Nguo za Mwanamke Mkristo

SEPTEMBER - MKIRI KRISTO BWANA WA MAISHA YAKO

Mkiri Kristo Bwana wa Maisha Yako kama Mke
Mkiri Kristo Bwana wa Maisha Yako kama Mama
Mkiri Kristo Bwana wa Maisha Yako kama Jirani
Mkiri Kristo Bwana wa Maisha Yako kama Mshiriki wa Kanisa

JULAI, 1967

MPANGO WA KWANZA

HURU KUTOKA KWA SHERIA!

Wimbo: Alisulibiwa Yesu

Maandiko Matakatiifu: Wagalatia 5:1-21

Ombi

Wimbo: Deni Yangu ya Dhambi

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Mwezi huu, tutafikiri sote pamoja juu ya 'Ukristo Dhahiri' Somo hili la kwanza, tutajifunza pamoja kwa uangalifu, Wagalatia 5:1-21. Na halafu, katika masomo matatu yafuatayo tutajifunza kwa uangalifu Wagalatia 5:22 na 23. Tafadhali ufunue Biblia yako sasa wakati nisomapo (au omba mtu fulani kusoma wakati wanawake wote wanafuata kusoma Maandiko Matakatiifu katika Biblia zao) Wagalatia 5:1-21.

Sehemu ya I: Historia Fupi ya Kitabu cha Wagalatia: (Katika Biblia ya Kiswahili, kunazo ramani katika nyuma ya Biblia. Kwenye ramani ya mwisho, 'Ulimwengu zamani za Agano Jipya', utaona nchi ya 'Galatia'. Onyesha Wanawake Galatia.) Mmisheni Paulo aliandika kitabu cha Wagalatia, kwa watu wa Galatia, karibu mwaka wa 60 A.D. Pengine kiliandikwa kwenye safari ya tatu ya mmisheni Paulo wakati alipokuwa kwenye mji mkuu wa Korintho (Onyesha wengine mji huu mkuu kwenye ramani ile ile).

Makundi makubwa, wengi wao wakiwa sio Wayahudi, walikuwa wame-mkiri Kristo katika Galatia, kwa sababu ya kazi ya Paulo. Wakati mwingine baada Paulo alikuwa ametoka Galatia, waalimu Wayahudi fulani walifika wakinena kwa nguvu ya kwamba watu wasio Wayahudi hawatakuwa Wakristo bila kuzifuata Sheria za Musa, kama ilivyoandikwa mbele katika vitabu vya kwanza vya Agano la Kale. Watu wa Galatia waliweka usikivu kwa mafu-

ndisho haya, jinsi walivyofanya mara ya kwanza wakati walipoupokea ujumbe wa Paulo juu ya wokovu katika Yesu Kristo. Kulikuwako na enezi la tohara miongoni mwa Wakristo wasio Wayahudi. Tohara ni jina la Jando katika desturi za Yuda. Paulo alisikia juu ya vitendo hivi.

Na kwa hivyo, Paulo aliandika barua hii kwa watu wa Galatia, kueleza kwamba tohara, ingawa ilikuwa sehemu inayohitajika ya Maisha ya Taifa ya Kiyahudi; haikuwa sehemu ya Injili ya Kristo na haikuwa na kitu cho chote hata kidogo kuhusu Wokovu.

Sehemu ya II: Kuwekwa Huru na Kristo kutoka Utumwani wa Sheria
(Gal. 5:13, 14, 15).

Tunahitaji kujua bila wasiwasi, kwamba tukiwa waamini katika Bwana Yesu Kristo, tuna huru kutoka kwa dhambi na Sheria. (Soma Yohana 5:24 na Warumi 8:1 na 2). Mkristo hayuko chini ya Sheria, lakini chini ya neema (Warumi 6:14).

Mwamini amezaliwa kutoka juu; maana yake ni kutoka kwa Mungu, na kwa hiyo anayo asili mpya ya Mungu. Roho Mtakatifu anaishi katika moyo wa kila mwamini. Ana uhuru katika Kristo Yesu.

Kitu ambacho tunahitaji kusema na kusema mara tena, kujifunza na kuamini kweli mioyoni mwetu kama waamini kwa Bwana Yesu Kristo, ni neno hili la kweli kutoka katika Maandiko Matakatifu: Mwamini halazimishwi na Sheria, lakini na upendo, kwa maana 'pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepeleka sisi'. (Rum. 5:5).

Sehemu ya III: Kazi za Mwili

Ebu tuangalie tena, katika Wagalatia 5:19-21. Vifungu vya Maandiko Matakatifu hivi vinasema juu ya matendo ya mwili. Mwishoni Paulo hakutaka kuacha nafasi ya yote hapa kwa kukosa kufahamu. Anataja dhambi maalum za mwili. Matendo ya mwili hayafichwi na siri—yamejulikana! Kwanza zimewekwa orodhani 'dhambi za mwili' — ambazo zimefanywa kwa ana-

ni jinsi Yesu anaweza kuongoza mapito yetu. Lazima tuwe jinsi Yesu angekuwa na Atatuonyesha kile tunapaswa kufanya.

Mwisho: Mwezi huu tumefikiria juu ya kumkiri Kristo kama Bwana wa maisha yetu katika hali yetu ya wake, jirani na washiriki wa kanisa. Kwa jinsi hivyo twaona kwamba sisi wanawake lazima tuweke tumaini letu katika Kristo kila sehemu ya maisha yetu. Ni lazima tuonyeshe Kristo katika maisha yetu kila mahali. Hebu sote tujifunze Mithali 3:5-6, ili kwamba tunapoonza kwamba tutafanya machache kuliko yale Yesu anataka sisi kufanya tutaweza kukisema kifungu hiki na kufanya zaidi.

Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako'.

Sehemu ya II: 'Usizitegemee Akili zako mwenyewe'

Wakati washiriki wa kanisa wanapotegemea mawazo na matendo yao wenyewe huwa njia ya wanadamu badala ya Bwana. Mara nyingi huwako tatizo kweli au hitaji kanisani. Labda washiriki wa kanisa wanajisikia kwa Mkristo mwingine amefanya tendo la dhambi. Sisi washiriki wa kanisa tukifanya vile 'sisi' tufikirialo ndilo laweza kufanyika kila mara lita-kuwa kosa. Lazima tuombe na kutegemea akili za Mungu. Bwana anajua mengi zaidi kuhusu kanisa Lake na ikiwa sisi Wakristo tutaonyesha kwamba kweli tunamtegemea Bwana, makanisa yetu yatakuwa jinsi Kristo apendavyo yawe.

Sehemu ya III: 'Katika njia zako zote mkiri yeye'

Wakristo ambao ni washiriki wa kanisa wana njia maalum ya kuonyesha watu ambao hawamjui Yesu maana ya kuwa mshiriki wa kanisa. Njia maalum hii ni kwa kuweka tumaini letu katika Yesu katika mambo yote tufanyayo. Katika nyumba zetu, sokoni, tunapowazuru jirani, na katika kazi yetu ya kanisa, tunataka kuonyesha upendo wetu na tumaini kwa Kristo. Twajua hatuwezi kuwa kama Kristo wakati wa kuwapo kanisani tu kwa sababu watu hutuambia mahali po pote tulipo. Kujaribu kumfuata Yesu kanisani na kisha kumwacha Yesu wakati tunachapo kanisani kunawaonyesha wale karibu nasi kwamba hatumfahamu Yesu kamili wala kumpenda hata kidogo. Ni lazima tumkiri katika njia zetu zote.

Sehemu ya IV: 'Naye atayanyosha mapito yako'

Ikiwa sisi washiriki wa kanisa tunaweza kuweka maisha yetu katika Kristo, ikiwa tutampokea Kristo kuwa Mrokozi wetu itakuwa rahisi kumtumaini Bwana kwa moyo wetu wote. Hatutapenda kuzitegemea akili yetu yenyewe kwa vile tutataka Kristo atuongoze. Tutapenda kumkiri Kristo katika yote tutakayofanya. Ikiwa tutafanya vitu hivi tunajua Kristo ataongoza hatua zetu. Mkristo mmoja aliandika kitabu kiitwacho KATIKA HATUA ZAKE. Hadithi hii ni juu ya Mkristo ambaye alijaribu kufikiri vile Kristo angefanya kabla ya kufanya kitu cho chote. Alijaribu kutembea katika hatua za Yesu. Alijaribu kuwa kama Kristo angekuwa. Hii

sa za mwili na tamaa. Dhambi hizi kama zilivyotajwa katika maana ya maneno haya yote.)

Tena Dhambi za Ushirikina' zimetajwa katika Wagalatia 5:20 Ibada ya sanamu na Uchawi. Kwa ufupi jadilia juu ya dhambi hizi mbili na maana yake!

Kwenye orodha ifuatayo tena ni 'Dhambi za Tabia' vile vile kutoka katika Wagalatia 5:20: Uadui, Ugomvi, Wivu, Hasira, Fitina, Faraka, Uzushi na Husuda. Tena, hakikisha kwamba wanawake wana maana ya kweli ya kila moja ya maneno haya.

Mwishowe, kuna orodha ya Dhambi za Kupita Kiasi' katika Wagalatia 5:21. Hizi ni ulevi na Ulafi. Jadilieni mambo haya mawili.

Lazima hapa tufahamu, kwamba Wakristo watatenda moja au mengi ya 'Matendo ya mwili', lakini mwamini wa kweli katika Yesu hatakuwa na furaha kuendelea kutenda dhambi hizi. Angalia katika Neno la Mungu katika Wagalatia 5:22 'Linamaje juu ya wale ambao wanaendelea katika dhambi hizi? Hawataarithi ufalme wa Mungu.' Hawataokolewa.

Mwisho: Hii inamaliza mpango kwa leo. Soma tena, Wagalatia 5 kabla ya wiki ijayo. Itakuwa vizuri kusoma kitabu chote cha Wagalatia, na jadiliana na mwamini mwingine, kifungu cho chote cha Maandiko Matakatifu ambayo huelewi.

JULAI, 1967

MPANGO WA PILI

TUNDA LA ROHO: UPENDO, FURAHA, AMANI

Wimbo: Anekombolewa na Yesu

Maandiko Matakatiifu: Wagalatia 5:16, 18, 22, 23.

Ombi

Wimbo: Nijaze Rwanangu

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Wiki iliyopita, tulimaliza mpango wetu, tukizungumza juu ya matendo ya mwili jinsi ilivyotajwa katika Wagalatia 5:19, 20, na 21. Tunaanza wiki hii kwa kuzungumza juu ya tunda la Roho. Katika Wagalatia 5:22 na 23 yametajwa matokeo tisa ya tunda la Roho. Neno lenyewe siyo matunda bali ni tunda. Kama vile mti wa mchungwa huwa na machungwa mengine, hatusemi matunda ya mti wa mchungwa bali husema tunda.

(Soma Wagalatia 2:20). Kwanza ni lazima pawepo na shauku ndani ya moyo wa mwamini ndipo tunda hili la Roho litaonekana katika maisha yake. Hii yawezekana kwa sababu ya muungano wa maisha ya Mwamini na ni tunda nzima la Roho kwa wale ambao wamejitoe kwake. (Soma Yohana 15:5). Tunda la Roho ambalo tutazungumza juu yake leo lalinganishwa na hali ya ndani ya mwamini.

Sehemu ya I: Upendo

Ni vema mno hata tunda la Roho la kwanza lililotajwa ni upendo. Tunaanza na tunda lililo zuri, tena lililoiva sana, na kuendelea mpaka kwa lile bila mapambo na gumu. Neno Upendo lingeweza kuwa neno lenye nguvu sana lililotumiwa katika Biblia. Mpende jirani yako kama nafsi yako. 'Pendeni,' Mungu wa upendo atakuwa pamoja nanyi,' 'upendo wa Kristo,' na tunaweza kuendelea zaidi na zaidi kazi ya Mkristo ya upendo

SEPTEMBER, 1967

MPANGO WA NNE

MKIRI KRISTO BWANA WA MAISHA AKO KAMA MSHIRIKI WA KANISA

Wimbo: Katika Neema ya Yesu

Maandiko Matakatiifu: Mithali 3:5-6; Waefeso 5:23-27

Ombi

Wimbo: Mteteeni Yesu

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Tukiangalia katika maandiko ya Biblia twajua kwamba Kristo alilipenda kanisa. Yesu alitupenda sana hata akatoa maisha yake kwa ajili yetu. Njia ambayo tunayo ya kujaribu kusaidia watu wote kujua upendo wa Kristo ni kwa njia ya kanisa. Wengi wetu ni washiriki wa kanisa. Sisi tu sehemu ya kundi ambao tunaona kuwa ni wajibu wetu kuwasaidia watu wengine kumjua Yesu. Tutawezaje kuwa sehemu ya kanisa ambalo Kristo alilipenda?

Sehemu ya I: Kutafuta Pamoja kwa Moyo wako wote'

Mojawapo ya vitu vya kwanza ambavyo Wakristo wanaonyesha katika maisha yao ni imani wanayo katika Bwana. Watu ambao si Wakristo wanaendelea katika maisha yao wakijaribu kutafuta kitu chenye maana. Sisi Wakristo na washiriki wa kanisa tunayo kazi ya kuishi imani tuliyo nayo katika Kristo kila siku. Biblia yasema 'Mtumaini Bwana kwa Moyo wako Wote'. Tunafahamu tofauti ya kuwapenda watoto wa marafiki wetu na upendo tunao kwa watoto wetu wenyewe. Upendo tunao kwa watoto wetu wenyewe uko na moyo wetu wote. Hii ni aina ya tumaini ambalo sisi washiriki wa kanisa lazima tuwe nalo katika Bwana kwa moyo wetu wote.

Esther: Nilianza kuomba zaidi kuhusu hii na nilijisikia Yesu anitaka nijifanye kuwa rafiki kwa mama yule. Nilipoanza kumtembelea alianza kuja nyumbani kwangu. Kwa upesi alikuwa akiniomba kumsaidia kujifunza kupika na kusafisha. Nilimtegemea Bwana kunifundisha ili niwe rafiki yake. Hii ilichukua wakati, lakini halafu alianza kwenda kanisani pamoja nami. Mchungaji alikuwa akizuru nyumbani kwake na kumshuhudia mume wake. Bwana aliyanyosha mapito yetu na tuliweza kuwaona jamaa hawa wakiwa wenye furaha.

Mary: Nakipenda kifungu hicho, Esther. Tofauti katika njia uliyokuwa jirani na katika njia tuliyomo kwa kawaida ni hili: ulimtumaini Yesu na moyo wako wote. Hii ni muhimu kweli kweli. Ikiwa tunatumaini katika Yesu kwa moyo wetu wote itakuwa rahisi kwa Yesu kutuonyesha ni nani jirani zetu na jinsi anavyotaka tuwasaidie.

Ruth: Njia yetu bora ya kuwasaidia ni kuwassaidia waje kumjua Yesu kama Bwana wa maisha yao. Ikiwa tunaishi karibu na Kristo ni rahisi kwa marafiki zetu na jirani kuona na kupenda kumjua Yesu wetu. Itakuwa bora tukijifunza Mithali 3:5,6 moyoni mwetu, ili kwamba tuweze kufikiri juu ya hitaji letu la kumweka Kristo kwanza.

Ombi: Omba kwamba tutankiri Kristo kama Bwana wa maisha yetu kama jirani.

— huwa na mipaka? La. Wanawake vijana na wanawake wazee wanapaswa kuwapenda waume wao. (Soma Tito 2:4); wazazi wanaambiwa wawapende watoto wao. (Soma Tito 2:4); Wanaristo wanawazwa kuwapenda adui wao (Mathayo 5:44); tunapaswa kuipenda Biblia (Zaburi 119:97); na tunapaswa kulipenda kanisa (Zaburi 26:9). Katika maisha yote, kama waamini, tunapaswa kuonyesha upendo wa Mungu katika mioyo yetu.

Sehemu ya II: Furaha

Furaha ya kweli ni tunda lingine la maisha yaliyojazwa na Roho. Mwanamke mmoja mchaji wa Mungu alikuwa katika hali ya kufa. Majenzi yalipokuwa yakitiririka, dada yake aliinama karibu naye na akanwambia 'Kilio chaweza kuendelea kwa usiku lakini furaha huja asubuhi.' (kutoka Zaburi 30:5). Aliyekuwa akitaabika alifungua macho yake na kusema 'Furaha sasa!' Tata katika maumivu makali alikuwa na furaha ambayo ni tunda la Roho.

Sehemu ya III: Amani

Hatuishi katika ulimwengu wenye amani, lakini twaweza kuwa na amani pamoja na Mungu na kuishi katika amani na watu wengine. Kweli, tutakiwa waamini, tunaweza kuwa na amani ipitayo ufahamu wote' katika mioyo yetu kila siku.

Mwisho: Soma tena kabla ya wiki ijayo mlango wote wa Wagalatia 5.

JULAI 1967

MPANGO WA TATU

TABIA MBELE YA BINADAMU NA MUNGU

Wimbo: Katika Neema ya Yesu
Maandiko Matakatiifu: Wagalatia 5:22 na 23
Omba
Wimbo: Yesu Kwetu ni Rafiki
Kutaja Majina
Shughuli
Mpango

Utangulizi: Wiki iliyopita, tulijifunza juu ya tunda la roho la upendo, furaha na amani. Leo katika mpango wetu, tutajifunza juu ya tunda la Roho lililoonyeshwa mbele ya wanadamu na Mungu.

Sehemu ya I: Hebu tujadilie kwa ufupi, maana ya maneno uvumilivu, wema, na fadhili, na kuhakikisha ya kwamba tuna ufahamu wa kila neno.

Uvumilivu ni kinyume cha kukasirika upesi. Mkristo yu tayari kuvumilia udhalimu au mzaha. Imani yake haiwezi kuharibika na vitu vya ulimwengu vinavyoonekana. Atavivumilia kama askari mzuri wa Yesu Kristo. Anajua ya kwamba ingawa adui zake watawumiza kwa mwili hawataweza kugusa roho yake. Atavivumilia vile vile kwa sababu ya upendo katika moyo wake na tamaa ya kuwaona wadhalimu wake wakija kwa Mwokozi. Hatakata tamaa katika juhudi zake kuwaonyesha upendo wa Mwokozi.

Utu wema maana yake ni kwamba uzuri wa Mkristo si nje ya mwili tu ili kwamba wengine waone vitendo vyake vizuri na kumsifu. Uzuri wake uko ndani yake. Haidhuru kwake kama akipokea sifa ya binadamu. Amekusudiwa kutoka ndani ya kutenda vitendo vizuri na kusema juu ya mambo manyofu. Hakuna dhambi ambazo zimefichwa katika maisha yake. Ametakaswa na Mungu.

kaniomba niende kumzuru mwanamke ambaye alikuwa na watoto wagonjwa. Hakuishi karibu nami na sikukuwa na hakika kwamba nilipaswa kwenda kwa vile hakuwa wa kabila langu. Mchungaji alinisomea hadithi ile kutoka Luka na alinisaidia kuona ya kwamba lazima niende kumsaidia mwanamke huyu kama Msamaria alimsaidia mtu aliyeumizwa. Jirani zangu ni watoto wa Mungu maana yake ni kila mtu.

Esther: Hii ni kweli, Ruth. Lakini pengine si rahisi kuwapenda kama tutajipendavyo sisi wenyewe. Kulikuwako na jamaa walioishi karibu nami ambao sikuweza kuwapenda. Mama hakuonekana mwenye kujali kuwatunza watoto wake au nyumba yake. Baba alikuwa akinywa pombe na halafu kupiga kelele kwa jamaa zake. Kijana wake alikuwa na taabu na polisi kwa kuiba. Niliwezaje kupenda watu hawa kama ninavyojipenda mimi mwenyewe?

Mary: Hii ilikuwa vigumu. Ulifanya nini?

Esther: Kwanza niliomba juu yake. Siku moja wakati nilipokuwa nikisoma Biblia yangu nilisoma Mithali 3:5-6. Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote na Usizitegemee akili zako mwenyewe. Katika njia zako zote mkiri yeye naye atayanyosha mapito yako. Nilikata shauri kwamba napaswa kumtumaini Bwana ili anionyeshe jinsi ya kuwa jirani mwema na kusaidia jamaa hawa.

Mary: Unafikiri Yesu anakusudia kwamba tunapaswa kumtumaini Yeye katika mambo kama kuwa jirani mwema?

Esther: Ndivyo, Anafanya hivyo. Tangu nilipoanza kumwamini Yesu kuniionyesha kuwa jirani mwema nilianza kuona vitu vizuri kuhusu jirani zangu. Tangu nilipojifunza kuutegemea uwezo wa Yesu na siyo akili yangu mimi mwenyewe, ilikuwa rahisi kwangu kuwapenda jamaa hawa. Mwanamke alimwogopa mumewe. Ni kwa sababu hiyo hakuweza kufanya zaidi nyumbani. Walikaa katika kijiji cha kigeni na alijisikia na upekee.

Ruth: Sehemu nyingi ya yale maandiko matakatiifu yanasema Katika njia zako zote mkiri yeye Naye atayanyosha mapito yako. Ulifanyaje hii?

SEPTEMBER 1967

MPANGO WA TATU

MKIRI KRISTO BWANA WA MAISHA YAKO KAMA JIRANI

Wimbo: Mungu Ndiye Mwamba Wetu

Maandiko Matakatiifu: Mithali 3:5-6, Marko 12:30-31, Luka 10:25-37

Ombi

Wimbo: Deni Yangu ya Dhambi

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Tunataka leo kufikiri jinsi tunavyoweza kuonyesha kwamba Kristo ni Bwana wa maisha yetu katika njia ambayo tuishivyo na jirani zetu. Vifungu vya Biblia tulivyovisoma vinatufundisha sisi kwamba jirani wetu si mtu ambaye anaishi karibu nasi tu, wala wale wa kabila letu tu. Jirani zetu mara nyingi ni tofauti kutoka sisi. Sisi ni jirani wao kwa sababu tunaweza kuwajua jinsi tujipendavyo wenyewe—tunaweza kuwajua—na jinsi Kristo alivyotupenda sisi. Hebu niwajulishe Mary, Ruth, na Esther kwenu. Wawa ni wanawake watatu ambao watatusaidia sisi kufahamu mengi juu ya kumfanya Kristo Bwana wa maisha yetu kama jirani.

(Wanawake watatu ambao wanachukua sehemu katika mpango huu kama Mary, Ruth, na Esther wanapaswa kuketi mbele ya kundi kama wanavyotembelea katika nyumba ya Mary).

Mary: Nimekuwa nikisoma katika Biblia yangu kutoka katika Luka. Unajua hadithi ya mtu aliyemwuliza Yesu, 'Jirani yangu ni nani?' Vema, nimekuwa nikijaribu kufikiri—ni nani jirani wangu? Ruth, ni nani unayefikiria ni jirani wako?

Ruth: Kwa muda mrefu nilifikiri walikuwa ni wale wanaoishi katika kijiwa karibu nami. Watu ambao niliwaona kila siku. Halafu mchungaji wetu

Tunda lingine linakuja kama tokeo la uzuri wake wa ndani. Tunda hili ni fadhili. Mwanamke Mkristo anahusika na maisha ya watu wengine. Anajaribu kufahamu mahitaji yao na tamaa zao. Kwa fadhili anajaribu kuwasaidia. Ni mwangalifu asiye kusema maneno ya hasira ambayo yanaweza kumwumiza mtu mwingine.

Sehemu ya II: Imani ya mwanamke Mkristo iko katika Mungu. Yeye anajua ya kwamba amemwokoza na kwamba ana maisha tele ndani yake. Itiko lake kwa imani hii ni uaminifu. Kwa sababu ana imani katika Mungu na anafahamu kwamba habadili na hatasaliti imani ambayo ameweka ndani yake, yeye ni mwaminifu kwake. Uaminifu huu ni dhahiri katika hudhurio lake katika ibada za kanisa, katika mafundisho ya watoto wake nyumbani, na katika maisha yake ya usaidizi kwa marafiki na adui.

Upole ni tunda la Roho kwa sababu mwanamke Mkristo anajua ya kwamba pekee yake hana uwezo. Nguvu zake zote na mahitaji yake ya kila siku yanatoka kwa Mungu. Hawezi kujivuna kwa kitu cho chote. Kwa hivyo ni mpole. Katika upole wake kuna nguvu kwa sababu anauruhusu uwezo wa Mungu kufanya kazi katika yeye. Musa, mtu mpole sana duniani kote alikuwa mmojawapo wa viongozi wakubwa ulimwengu huu haujapata kuona.

Kiasi ni tunda ambalo linamwezesha Mkristo katika Roho Mtakatifu kuweza kutawala vile anavyoongea na kile anachoongea. Kiasi hutawala mambo ambayo anafikiria na jinsi ya kutenda.

Mwisho: Kama ikiwa Wakristo wote huzaa tunda la roho, ingekuwa tofauti la ajabu katika ulimwengu huu.

JULAI, 1967

MPANGO WA NNE

MAWAZO JUU YA WAGALATIA 5

Wimbo: Nitamshukuru Mungu

Maandiko: Jatakatifu

Omba

Wimbo: Yote Namtolea Yesu

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Mmisheni Paulo alifundisha wazi kwamba tukiwa waamini, hatufungwi chini ya Sheria. 'Tumeitwa kuwa huru'. Lakini, uhuru huu haukutafsiriwa kama ruhusa ya kutenda matendo maovu ya mwili (soma Warumi 6:1 na 2), kwa kuwa neema ambayo inatupa sisi uhuru vile vile inatupa asili mpya na uwezo katika Roho wa Mungu kuishi maisha ya kushinda dhambi za mwili.

Sehemu ya I: Kuishi katika Roho

Mkristo amepewa Roho (Soma 1 Kor. 6:19 na 20).

Wakati hawaamke anakuwa Mkristo, Roho wa Mungu anakuja kuishi ndani yake. Ni katika udongo wa Roho tu ambako tunda la Roho litakua. Katika Udongo wa mwili matendo ya mwili yatakua, lakini Mkristo ameitwa kuishi katika Roho kwa sababu ni katika Roho tu ambako tunda linaweza kukua, yaani upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. Tunda hili litadumu na kuendelea kuishi kwa sababu vitu vya kiroho ni vya milele. Matendo ya mwili hayataidumu jinsi mwili hautadumu. Maisha yetu katika Roho yatafanywa mazuri katika maisha yetu ya kila siku. Kwa kuwa tuna maisha, busara, na uwezo wa Roho, hebu sisi vile vile tutembeke katika Roho.

aye porojo au kusema maneno ya uwongo anaweza kujua kwamba ni rahisi kwa watoto wake kufanya vitu hivi vile vile kwa kuwa yeye ni mfano wa kuishi mbele yao. Mfano gani tunaishi kwa watoto wetu kufuata?

Sehemu ya IV: Naye atayanyosha mapito yako

Hakuna ye yote ambaye anahitaji uongozi mwingi kutoka kwa Mungu kuliko mama. Unataka kumkiri Kristo kama Bwana wa maisha yako. Yote ambayo lazima ufanye ni kumwamini Bwana kuokoa roho yako. Kusadiki kwamba wewe ni mwenye dhambi ni hatua ya kwanza. Kisha mwamini Yesu Kristo kukuokoa roho yako. Ukiamini hii Kristo atakuwa Bwana wa Maisha yako na atakuongoza katika mapito yako.

Omba: Omba kwamba tutatoa maisha yetu kwa Kristo na halafu kumwamini Yeye huyanyosha mapito yetu kuwa mama wazuri. Omba kwamba tutakuwa na shughuli ya kuwaongoza watoto wetu kuwa Wakristo.

kuwa ni nyumba ya mchungaji ni mfano kwa wengi. Akina mama wengi wa-naamini Bwana, lakini, je, twamwamini Yeye kweli na mioyo yetu yote? Sisi huweka mahali padogo ambapo ni kwetu kabisa. Tena tunaambiwa mara nyingi katika Biblia kutoa kwa Kristo maisha yetu yote na moyo wetu wote. Kuwa na nyumba kama hii ni lazima tufuate mfano wao na kuamini Bwana na moyo wetu wote. Tutoe moyo wetu wote kabisa kwa Yesu.

Sehemu ya II: 'Usizitegemee akili zako mwenyewe'

Kila mmoja wa watoto wetu anayo mahitaji yake mwenyewe. Mtoto mchanga lazima alishwe mara nyingi na asaidiwe zaidi. Yule mwenye umri wa miaka miwili anatumia tuzungumze naye, kuanza vile vile kumwambia juu ya upendo wa Yesu kwake. Mwenye miaka sita anataka kwenda shuleni, kujifunza kusoma na kuandika, na anataka kwenda kwa mama kwa usaidizi na kujua upendo wa mama na baba. Mwenye umri wa miaka kumi ni mzima kwa njia nyingi ingawa hata mtoto huyu anahitaji mama kumpenda na kujua jinsi ya kumsaidia. Hatuwezi kwa sisi wenyewe kujua kumsaidia kila mmoja wa watoto wetu. Wakati wanaposhindwa na shawishi na kusema uwongo tuna-wezaje kumsaidia mtoto kama huyu? Hatuwezi kuzitegemea akili zetu wenyewe. Lazima tuombe na kumwuliza Mungu kwa uongozi ili tuwe akina mama wema na kuwasaidia watoto wetu wakue kuwa wazima wa Kikristo.

Sehemu ya III: 'Katika njia zako zote mkiri yeye'

Madaraka makubwa ya mzazi Mkristo ni kumsaidia kila mtoto kumpe-nda Yesu na kumkiri yeye kama Mwokozi wake binafsi. Ikiwa sisi akina ma-ma tukifuata katika mambo yote mengine na tushindwe katika jambo hili tutakuwa tumeshindwa katika kazi ya mama. Watoto wanakaa na mama kuliko mtu mwingine ye yote. Ikiwa mama ni mtu mwenye furaha mtoto atajaribu kuwa vile kama yeye. Ikiwa yeye ni mwaminifu, akijifunza Biblia, kuomba mbele yao, akaenda kanisani na kuwapeleka watoto, hivi ni vitendo amba-vyo watoto watajaribu kufuata. Mtoto mdogo ambaye anahudhuria kanisani kwa kawaida atasikika akiimba nyimbo na mara nyingi atacheza 'kanisani'. Mama aliye Mkristo lazima awe mwangalifu kumkiri Kristo katika njia zake zote kwa kuwa watoto wake watamtazama na kuchungulia maisha yake. Mama ambaye anakunywa pombe, au kuvuta sigara, ambaye haendi kanisani; ato-

Sehemu ya II: Kutembea katika Roho

Maana ya hii ni nini? Kwa kweli maana yake ni:-

1. Kutoa wakati kila siku kwa masomo ya Biblia na ombi.
2. Kutoa sehemu ya pesa zetu na mali yetu kwa Mungu.
3. Kumshuhudia Kristo.
4. Utaratibu, utii na malezi nyumbani.
5. Ushirika na Wakristo wengine.
6. Kutafuta kusudi la Mungu kwa maisha yetu yenyewe.
7. Kumpa Kristo fahari katika vitu vyote.

Sehemu ya III: Wakati Mkristo aishipo katika Roho na kutembea katika Roho, hakuna nafasi kwa sifa-binafsi. Roho wa Mungu anafanya kazi. Yeye anajitoa kwake. Ikiwa mwanamke angelima shamba na apate kwekwe nyingi zimeanza kumea, hangekawia katika kuzing'oa kwekwe. Haitoshi kukata kwekwe tu kwa sababu zitaendelea kukua tena na zitazifinya mimea ambazo zimepandwa. Ikiwa tutakubali matendo ya mwili kukua katika maisha yetu, tunda la Roho halitakuwa na nafasi kuendelea. Tunda litafinywa. Hebu tuishi na kutembea katika Roho na kuzaa tunda kwa Bwana wetu.

Sehemu ya IV: Kwa kweli hili limekuwa funzo zuri kwetu sisi sote mwezi huu, kutoka Neno la Mungu. Tena, tunasoma kutoka katika Neno la Mungu, katika Mathayo 7:7, Maneno ya Yesu kwetu sisi, 'Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa.' Kama mmoja wetu akikosa mojawapo wa matunda tisa ya Roho, wacha tumwombe Bwana wetu kwa kweli, ambaye alisema, 'ombeni --- nanyi mtapewa'.

MPANGO WA KWANZA

MWANAMKE ANATOA SHAURI

Wimbo: 'Nataka Nimjue Yesu' Uk. 159 'Nyimbo za Sifa'

Maandiko Matakatiifu: 31:1-5

Ombi

Wimbo: 'Mungu Ulisema' Uk. 150 'Nyimbo za Sifa'

Kutaja Majina

Shughuli

Utangulizi kwa Mpango:

Mwezi huu tutajifunza juu ya mwanamke mwema katika Mithali 31). (Soma kifungu cha kwanza tena). Mnamo wakati ule Mama wa Mfalme alipo-chukuliwa kwa heshima kubwa kuliko mke wake. Tunapata majina ya Mama wa Mfalme mara nyingi katika Biblia. Kunao wanawake wengi wenye hekima ambao wametajwa katika Maandiko Matakatiifu: Miriamu, dada wa Mungu, Debo-ra nabii wa kike, Malkia wa Sheba, Huldah nabii wa Kike na wengineo. Si ajabu kusoma kwamba Mfalme Lemueli alimsikiliza mama wake.

Sehemu ya I: Katika kifungu cha 2 (Mwana wa nadhiri zangu' maana yake inaweza kuwa, 'mwana ambaye aliombewa katika ombi', kama Samweli (I Sam. 1:11) na kuwekwa wakf kwa Mungu, kama jina Lemueli linapodokeza. Maana yake inaweza kuwa 'uko katika nadhiri zangu za kila siku na maombi.' Ma-ma ambaye anawaomba watoto wake kila siku anatuambia kwamba anataka watoto wake kumtumikia Mungu na kwa kitendo hiki kwamba yuko karibu na Mungu.

Ingawa Lemueli alikuwa Mfalme, Mama yake hakuhusika na cheo chake lakini na afya yake binafsi na usafi wake. Anaambiwa asiache ma-isha yake, tabia, na vitendo vyake viongozwe na wanawake ambao ni waovu na wanaweza kuwaharibu wafalme na serikali.

MPANGO WA KWANZA

MKIRI KRISTO BWANA WA MAISHA YAKO KAMA MAMA

Wimbo: Bwana Mungu, Mashangaa

Maandiko Matakatiifu: Mithali 3:5-6, Zaburi 113:9

Ombi

Wimbo: Msalaba Nilipoona

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Wiki iliyopita tulifikiri juu ya tamaa yetu ya kuwa wake wazuri kwa kuamini katika Bwana. Wiki hii tunataka kufikiri juu ya maha-li petu nyumbani kama mama. Katika Zaburi 113:9, tunasoma kwamba Mungu anatufanya 'kuwa mama ya watoto mwenye furaha.' Watoto wako wana furaha tu kama mama anayo. Tukizuru nyumbani ambako mama ni mwenye furaha tuna-wapate watoto wenye furaha na wanaochekeka. Wakati mume au marafiki wana-pokuja katika nyumba hii wanakuwa wenye furaha vile vile. Yesu aliwapa furaha wote ambao aliwakuta wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Sasa tu-tafuata mfano wake na kuwapa furaha wale kando yetu. Tunawezaje kuwa mama wazuri na 'awe mama ya watoto wenye furaha'?

Sehemu ya I: 'Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote'

Kuna nyumba moja katika Dar es Salaam ambako ye yote apitaye anajua kwamba ni tofauti. Ni tofauti kwa sababu anajua ukienda humo Yesu anaishi pale. Hata wakati wa ugonjwa kungali na amani nyumbani na watoto wana furaha. Nyumba hii inaweza kuwa jinsi ilivyo kwa sababu mo-ja tu. Huyu mume na mke wanaamini katika Bwana kwa moyo yao yote. kwa

na tutakuwa wake wazuri. Tunajua ikiwa Kristo anatuongoza sisi tutakuwa wake wazuri jinsi tuwezavyo. Tutaimba wakati tufanyapo kazi yetu, kwa sababu tuna furaha. Tutaona ulimwengu mzuri wa Mungu, kwa sababu mioyo yetu inamfahamu Mungu. Tutaomba bila kukoma—tutakuwa katika hali ya ombi saa zote—kwa sababu tunampenda Yesu. Nampenda mwanamke kama huyu na mume wake atampenda vile vile.

Ombi: Ebu tuchungulie maisha yetu kuona ikiwa tunajaribu kuwa wake wazuri. Halafu ebu tuombe Mungu kutusaidia kufanya mazuri Kwake.

Ikiwa utakumbuka katika Agano Jipya mwanamke mwovu alidai kichwa cha Yohana Mbatizaji kwa sababu kucheza kwa binti wake kulimpendeza Mfalme.

Sehemu ya II: Mamaye Lemueli anamwambia (Kif. 4-5) kwamba kunywa mvinyo hakuwafai wafalme wa jamii ya kifalme. Katika Mithali anasema, 'Wakati kinywaji (au mvinyo) kinapoingia ndani siri hutoka nje.'

Katika kifungu cha 5 Mamaye anamwonya kwamba Mfalme ambaye amelewa anaweza kuisahau sheria ya kufanya makosa kwa sababu ya kutokuwa na fahamu ya kumwezesha kufikiri vizuri. Ni muhimu sana kwa watu ambao ni viongozi wa taifa kuwa na ufahamu bora saa zote. Rais, Mfalme au mjumbe wa serikali hawezi kuwa mwenye utumishi bora kwa watu wake akiendelea kunywa.

Sehemu ya III: Soma Mit. 23:29-35) Mvinyo wa nguvu unahusika na wana-wake kwa njia gani? Kila mlevi anawaambukiza wale wote wako karibu naye. Mume ambaye anatumia mvinyo hawezi kuwa mume au baba. Mara nyingi wana-wake na watoto wapate taabu kwa sababu pesa ambazo ziliweza kutumika kwa chakula, nguo, na ada ya shule, na mahitaji mengineo mengi ya maisha zimetumiwa kwa kunywa.

Majadilio: 1. Mwanamke Mkristo anapaswa kufanya nini akiambiwa kute-ngeneza pombe kwa mume wake na marafiki au kuwapa pombe? 2. Yeye anaweza kumjulisha mume wake na marafiki kwamba hataki kutengeneza pombe na kumwambia sababu yake? 3. Anapaswa kuomba marafiki zake Wakristo kumwomba mume wake? 4. Unawajua wanawake ambao wanakunywa na ambao wanahitaji ombi lako? 5. Mwanamke ambaye anatumia pombe anaweza kuishi halisi au atakuwa mlegevu katika maadili yake na pengine kuwa kahaba?

Mwisho: Omba kwamba Kristo aweze kuwashika walevi ambao unawajua. Washuhudie wale ambao wanahitaji Kristo. Omba kwamba utaweza kuwa mwenye nguvu katika mfano wake wa kuishi kwa ajili ya Kristo.

AGOSTI, 1967

MPANGO WA PILI

SHAURI LA MAMA JUU YA KUNYWA NA KUWASAIKIA MASKINI

Wimbo: 'Nyimbo za Sifa' Uk. 54 'Umechoka Hata Kuzimia?'

Maandiko Matakatiifu: Mithali 31:1-9

Ombi

Wimbo: 'Nyimbo za Sifa' Uk. 23 'Nina Raja Nawe'

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Mpango wa leo ni mfulizo wa mpango wa wiki iliyopita juu ya shauri lililotolewa na Mama wa Lemueli. Tunahitaji kufikiri leo jinsi tunavyoweza kuwasaidia wale karibu nasi katika matatizo yao. Tunawezaje kumsaidia mlevi, jamaa zake, wale wenye hitaji na wale katika huzuni.

Sehemu ya I: Ni katika miaka thelathini tu iliyopita tulipopata dawa nzuri. Watu ambao wanakufa na wale katika maumivu wanapewa dawa na madaktari kusaidia kuondoa maumivu.

Wanawake wa Yerusalemu waliwapa wahalifu waliokwenda mahali pa kifo kinywaji cha divai, ambacho kilipunguza maumivu. Hiki kilikuwa kinywaji ambacho kilikatazwa na Yesu, aliyetaka kuonja maumivu kamili ya kifo. (Mt. 27:34, Marko 15:23).

(Kif. 6) Kwa 'moyo mizito' maandiko matakatiifu haya maana yake ni wale walio katika huzuni. Wakati wa kifo cha mpendwa au jamaa wa ukoo au mmojawapo katika jamii, madaktari wanatoa dawa kutuliza yule ambaye yuko katika huzuni. Watu wa siku zile walikuwa na dawa ya aina moja tu. Ilikuwa mvinyo au mchanganyiko wa mvinyo na mimea ifaayo kwa dawa. Mithali 31:6 inazungumza juu ya utumizi wa kinywaji chenye nguvu kama dawa tu.

Sehemu ya II: 'Wala usizitegemee akili zako Mwenyewe'

Mke ambaye anataka kuwa mke mzuri anajua kwamba hawezi kufanya vizuri bila usaidizi kutoka kwa Mungu. Ufahamu wetu kila mara hautoshi. Hatujui ya kutosha; tunakasirika tunajiona. Lakini ikiwa tunamwamini Bwana na tusijitegemee wenyewe, hatutafanya makosa haya.

Rafiki Mwislamu aliniambia kwamba mume wake alikosa kurudi nyumbani kutoka kazini siku moja. Alikuwa kiongozi wa wawindaji wa wanyama wa porini. Hakurudi nyumbani kwa zaidi ya siku mbili. Mke alikuwa amekwenda kwa polisi, kwa mkuu wa kazi ya mume wake na kwa marafiki yake kujaribu kujua kwa nini mume wake hakurudi nyumbani. Kwa wanawake wote hii itakuwa vigumu lakini kwa Mkristo inafanywa rahisi kwa sababu hata tegemea ufahamu wake mwenyewe --- 'tunamtumaini Bwana.'

Sehemu ya III: 'Katika njia zako zote mkiri yeye'

Kwa wengi wetu ni rahisi kumkiri Mungu katika maombi yetu, katika kusoma Biblia yetu au wakati tuendapo kanisani. Biblia yetu inatufundisha kwamba inatupasa 'tumkiri Yeye---katika njia zote.' Mke anaweza kumkiri au kumwamini Mungu wakati apikapo, asafishapo nyumba yake, atengenezapo nguo za mumewe, na wakati awekapo mwili wake kwa usafi na wenyewe kuvuta. Ndavyo, anaweza kufanya hivyo na ni lazima. I Wathesalonike 5:17 inatufundisha sisi 'Ombeni bila kukoma.' Ikiwa 'Tunaomba bila kukoma' tutamwamini na kumkiri Kristo katika kila kitu. Mke ambaye anaiacha nyumba yake chafu, watoto wake bila kulindwa, chakula chake kutayari-shwa vibaya, nguo za mumewe chagu au bila kutengenezwa, mwili wake mwenyewe mchagu, hamkiri Kristo katika njia zote. Kwa sababu tunajua Kristo mioyoni mwetu inatupasa tumwonyeshe kwamba tunampenda Yeye na njia zetu.

Sehemu ya IV: 'Naye atayanyosha mapito yako'

Tulisema tunataka kuwa wake wazuri---wake ambao wanastahili mapenzi ya waume zetu. Wake ambao watawafanya waume zetu kutupenda zaidi. Ikiwa tumemwamini Kristo kumtegemea Yeye na si juu yetu wenyewe, kumkiri au kumwamini Yeye katika njia zetu hapo Kristo atayanyosha mapito yetu

SEPTEMBER, 1967

MPANGO WA KWANZA

MKIRI KRISTO BWANA WA MAISHA YAKO KAMA MKE

Wimbo: Baba, Mwana, Poho

Maandiko Matakatiifu: Mithali 3:5-6, Mithali 19:14

Ombi

Wimbo: Nitamshukuru Mungu

Kutaja Majina

Shughuli

mpango

Utangulizi: Katika vifungu vingi tunafahamu Yesu alifundisha kwamba mume ampende mke wake. Kol. 3:18, 1 Petro 3:1, Efe. 5:25 ni vichache vya hivi. Ikiwa mume atampenda mke wake mke lazima astahili mapenzi yake. Katika Mithali 19:14 tunasoma kwamba Nyumba na mali ni urithi apatao mtu kwa babaye. Tunajua ya kwamba baba mara nyingi anamsaidia mwana wake kuanza maisha yake, kupata elimu yake na njia ya kuishi. Lakini ikiwa mke ni mke mzuri huyu ni zawadi ya Mungu. Mke mwenye busara, mtu hupewa na Bwana. Leo ebu tufikiri jinsi tuwezavyo kabisa kuwa wanawake wazuri.

Sehemu ya I: Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote'

Kila asubuhi tuamkapo tunahitaji kukaa kimya dakika chache na kuzungumza kwa Mungu. Hii hutusaidia kuendelea siku nzima tukiwa na uwezo wa 'Kumtegemea Bwana.' Wakati shida zinapotuangalia kwa haraka tunamwamini Mungu. Ikiwa tunaweza kuwa wanawake wema, aina ambayo wanaume zetu wanaweza kupenda, ni lazima tumwamini Mungu na vitu vidogo. Bila ombi hatuwezi kabisa kumwamini Bwana. Wengi wa wanawake katika makani yetu wanaolewa na wanaume ambao si Wakristo. Kwa wanawake hao ni wajibu wao kuomba na kumwamini Bwana kuwaokoa waume zao. Ni wajibu wa mke kuomba kila siku—hata kwa miaka mingi mpaka mume wake ameokolewa.

Sehemu ya II: Katika kifungu cha 7 Mamaye Lemueli anasema, 'Isingwe wewe mwenyewe lakini mpe mtu maskini ili asiikumbuke tena taabu yake'. Je, hii ingeweza kuwa ya usaidizi kwa ye yote mwenye hitaji? Mtu atahitaji kulewa kabisa ili kusahau matatizo yake yote. Hii haiwezi kuondoa tatizo. Mtu hawezi kufanya kazi akiwa katika hali ya ulevi kwa hivyo matatizo yake yatakuwa mengi akinywa.

Sehemu ya III: (Kif. 8-9) Kusema juu ya bubu maana yake ni mtu ye yote ambaye kwa sababu fulani hawezi kunena mwenyewe. Labda yu mtoto sana, mwoga, mjinga au asiyejua kitu. Mfalme amesisitizwa kuamua vyema na kuwasaidia wale maskini na watu wenye hitaji.

Mwisho: (Soma Kif. 20) Wakiwa kundi la Wanawake mnaweza kumsaidia ye yote ambaye ni maskini na mwenye hitaji. Unaweza kusema, 'Mimi mwenyewe niko katika hitaji.' Katika matoleo yetu ambayo tunachukua kila wiki tunaweza kuamua kile tunahitaji kufanya na pesa hizi na kukifanya katika jina la Kristo. Ikiwa unaishi katika jamii ya walimaji na unamjua mtu fulani asiyekuwa na chakula, pengine kila mmoja ataleta mboga kumsaidia yule mtu au jamaa zake. Wakati mwingine wazee wanaachwa bila mtu ye yote wa kuwatunza. Huu si wajibu wako kumsaidia yeye?

Ni desturi katika mahali pengi kuchukua chakula kilichopikwa nyumbani ambako kifo kimetokea kumsaidia kuwalisha wageni wote na jamaa. Hiki ni kitu ambacho wewe peke yako au pamoja na wengine unaweza kufanya kuonyesha uhusiano kwao na upendo wako kwa Kristo.

Ombi: Omba kwamba tunahusika na kufanya kitu kwa wale karibu nasi.

AGOSTI, 1967

MPANGO WA TATU

VITENDO VYA MWANAMKE MWEMA

Wimbo: Nyimbo za Sifa' Uk. 161 'Ni Wako Wewe'
Maandiko Matakatiifu: Mithali 31:10-31
Wimbo: Nyimbo za Sifa' Uk. 58 'Yote Namtolea Yesu'
Kutaja Majina
Shughuli

Utangulizi: Katika maandiko matakatiifu ya leo tunaona mwanamke Mkristo mkamilifu akiishi aina ya maisha ambayo tungependa kufuata. Anayo sifa yote ambayo mwanaume anahitaji katika mke. Atamfanya mwanamke ye yote kujisifu kuwa naye kama binti au mke. Yeye ni mwanamke mpole, msafi, mwenye bidii, mkarimu na ana hekima. Anashiriki na wale wasiokuwa na baraka. Leo tutasoma nusu ya funzo hili na wiki ijayo nusu nyingine.

Sehemu ya Kwanza: (Kif. 10) Ikiwa mwanaume angekuwa akimtafuta mke katika Afrika ya Mashariki na angesikia sifa nzuri kama hii angemwambia baba yake na jamaa zake wengine, 'Nisaidie kuchanga pesa ili niweze kulipa mahari kwa mwanamke huyu. Ninazo shilingi elfu moja na uzuri wake ni zaidi ya bei ya ng'ombe kumi nzuri pamoja na shilingi zangu elfu moja na utajiri wote nitakaoweza kumpa baba yake.' Maandiko Matakatiifu yanasema kima chake chapita kima cha marijani.

Sehemu ya II: (kif. 11) Mwanamke huyu aliweza kuaminiwa na pesa ambazo alipewa kununua chakula, nguo na vitu vingine vinavyohitajiwa nyumbani. Hakutumia pesa bure kwa vitu visivyo vya maana au kuzitumia pesa zote mara moja. Mke mzuri ambaye amepewa pesa kwa matumizi ya nyumba kwa jamaa anapaswa kupanga jinsi ya kuzitumia kwa njia nzuri. Hapaswa kukimbia dukani na kununua mito ya kichwani, mifuko ya mito ya kichwani, shuka za kitanda, na nguo mpya kwa kila mmoja na halafu kuwaacha jamaa zake kubaki bila chakula kwa sababu amezitumia pesa za mumewe kwa njia mbaya.

Sehemu ya IV: Tunaweza kuvaa nguo za siku hizi bila kuwa wachafu au wenyewe kukosa adabu. Wamalaya katika miji mikubwa na mahali pengine wanavaa nguo fupi, na zinazokaza miili yao kuonyesha wazi miili yao ili kuwavuta wanaume katika kazi yao. Hakuna mume ambaye anapenda bibi yake kuvaa kwa njia hii. Kuna tofauti katika kuvaa nguo iliyonyoka (yaani ya taiti) ambayo inatosha vizuri na ndefu ya kutosha kuwa stahivu na kuvaa nguo ambayo imekaza sana ili mshono wake unataka kupasuka na fupi sana ili karibu mwili wako wote unaonekana. Wanawake wanafanya dhambi kwa kuvaa nguo ndogo sana na zenye kudhihirisha sana.

Nguo na mapambo ambayo ni mema kuvaa katika kabila moja au jamii yatakuwa mabaya katika kabila lingine. Kwa kawaida wanawake wa Kikuyu ambao wanakuwa Wakristo wanaweka mbali shuka zao na pete za sikio kwa sababu hizo ni alama ya ushenzi. Wanataka wengine kujua kwamba wanaziacha njia za kizamani na kumfuata Kristo. Vitu vya dhahabu au mapambo yanafikiriwa kama hirizi au ikiwa vitu hivi vina imani ya uramali inayohusiana navyo ni vibaya. Hakuna ubaya kwa kuvaa vitu vya dhahabu ikiwa hivi si hirizi. Kuvaa mapambo mengi si vizuri kwa Mwanamke Mkristo. Nguo zo zote au vitu vya dhahabu ambavyo vinapunguza ushuhuda wako wa Kikristo ni vibaya.

Sehemu ya V: Soma 1 Petro 3-5 Hakuna ubaya katika kuisuka nywele, kuichanua, au kuinyosha. Katika kifungu cha tatu kinasema usiwe na kiburi na kutaka kutumia nafasi yako yote kujaribu kufanya nywele yako kuwa malidadi kwa kuweka mapambano kutaka kuvaa mavazi mapya na ya kupendeza wakati wote. 'Upendo wa mwanamke wa mapambo ni mzizi wa maovu yote, si kidogo kuliko upendo wa mwanamume na pesa.'

Katika kifungu cha nne badala ya mapenzi ya mapambo ya nje inatupasa tujipambe wenyewe na uvumilivu na upole. Vitu vilivyofichwa moyoni haviwezi kuharibika.

Mwisho: Ongea habari za nguo zinazofaa kuvaa katika jamii yako na kwa nini. Vitu gani haviwezi kuvaliwa kwa sababu ya imani ya uramali? Mapambo gani na nguo unapaswa kuepukana nazo kwa sababu wewe ni mwanamke Mkristo?

nguo zilitengenezwa kwa mikono zamani sana kabla ya mtu kuwa na akili kutosha kuvumbua cherehani. Baada ya kukusanya vyombo vyako hautapata taabu ya kumpata mtu wa kukufundisha. Kwa kufanya hivi unaweza kuwasaidia jamaa zako na tena marafiki zako. Kwa kushona unaweza kuweka pesa ambazo ungempliwa fundi wa cherehani.

Sehemu ya II: (Vif. 23+28) Mwanamke ambaye ni Mama mwema, mke mwema na mtunzaji mzuri wa nyumba anafahamika upesi na wale katika jamii. Kuwa msafi tu, mpikaji, na kushona nguo havitoshi. Katika kifungu cha 25 kinasema, 'Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake.' Mwanamke Mkristo ambaye anafahamika maisha yake vizuri kama awezavyo na kufanya wajibu wake vizuri kama ajuavyo hataogopa katika wakati wa uzee wake.

Mwanamke ambaye amefuata mafundisho ya Biblia ataweza kuzungumza na hekima na fadhili anapokua katika maisha ya Kikristo na anapokonga.

Hakuna mmoja ambaye atasimama na kumsifu mwanamke mlegevu wala mume wake na watoto wake hawatamheshimu.

Sehemu ya III: (Kif. 29) Pengine hii hutafsiriwa kuwa maana yake, 'binti wengi wamepata utajiri' au 'wengi wamefanya vizuri lakini wewe ume-fanya zaidi.' Hatuwezi kuwa matajiri sote wala wakamilifu lakini tuna-weza kufanya vizuri tuwezavyo na vile tulivyo navyo. Tajiri au maskini tuna nafasi sawasawa kuwa wazuri.

(kif. 30) Tuna misemo miwili katika Amerika, 'Urembo ni ngozi tu' na 'Sura nzuri ni kama mwenye sura nzuri afanyavyo'. Je, umejua mtu mwenye sura mbaya sana ambaye sura yake ilionekana nzuri baada ya muda fulani kwa sababu ya urembo ndani yake. Alikuwa na maadili mengi tumekuwa tukizungumza juu yake na ulisahau kwa haraka kwamba alikuwa mwenye sura mbaya. Bila shaka umewaona wanawake ambao walikuwa warembo kuwa-angalia lakini baada ya kuwajua wanapoteza urembo wao kwa sababu walikuwa wachoyo, walifikiri juu yao wenyewe; hawakupenda kuwasaidia wengine; walisema vitu vibaya juu ya kila mtu. Mwanamke mrembo anaweza kuharibu sura yake kwa vitendo vyake vibaya.

Kwanza anapaswa kupanga ni kiasi gani cha chakula cha mahindi kitahitajika, mafuta ya kupikia, sukari, chai, unga, maharagwe, chumvi bizari, sabuni, mchele na vyakula vinginevyo vya kawaida watakatavyotumia kwa mwezi mzima. Baada ya kuvinunua vyakula hivi vya kawaida atafikiria ni pesa ngapi amahitaji kuweka kutumia kwa maziwa, matunda, mboga na ikiwezekana nyama ikiwa atakuwa na pesa ya kutosha kuinunua. Kitakachofuata ni kufikiria ni mtu gani anahitaji gauni, au shati, au nguo zinginezo ambazo zinahitajika na ipi ni ya muhimu sana kununuliwa. Akiba ya pesa chache kila mwezi kwa kero ya shule ni kitu kizuri kukumbuka. Mabwana wengi wangekubali kuwapa mabibi zao pesa wangewaonyesha kwamba wanajua jinsi ya kuweka pesa na kutokuwa waharibifu wa pesa.

Sehemu ya III: Mara nyingi katika mji mkuu wanawake wengi wanaketi tu kama hawana kitu cha kufanya. Ikiwa ungeingia katika nyumba zao pengine ungeona kwamba wanaweza kuisafisha milango, madirisha, kuta za nyumba, vifaa vya nyumba, na nguo zao, matandiko ya kitanda, watoto na vitu vinginevyo vingi ungeweza kutaja. Ni furaha kwa bwana kurudi nyumbani kwenye nyumba safi, watoto wasafi na mke msafi.

Bibi mzuri ataamka mapema sana na kuona juu ya chakula cha siku. (kif. 15) Ikiwa mume wake na watoto wa shule wanapaswa kuondoka nyumbani mchana kutwa atawatayarisha chakula cha kubeba. Ikiwa ana pesa kutosha anaweza kutayarisha chupa ya chai kwa mume wake na maziwa kwa watoto. Mume ambaye amelishwa vema atafanya kazi vizuri na kujisikia vizuri. Mtoto hawezi kusoma vizuri akiwa na njaa.

Sehemu ya IV: Ni mwanamke gani ambaye atakuwa na faida yote angekuwa na shamba na angeliacha kumelea kwekwe badala ya kupanda mboga kuwalisha jamaa zake? Katika kifungu cha 16 mwanamke anafikiri juu ya shamba na halafu kulinunua na kupanda kile alichofikiri kitamea vizuri.

Katika kifungu cha 17 kunaeleza nguvu na juhudi ambayo anajitayarisha nayo kufanya kazi. Mwanamke anahitaji kuamka na kuingia shambani mapema na kufanya kazi kabla jua halijakuwa kali. Anapaswa kutumia sehemu ya jua kali ya siku kwa kusafisha nyumba na kusafisha nguo. Wakati inapokuwa tulivu anaweza kurudi shambani mwake.

(kif. 18) Hata usiku mwanamke huyu anashughulika kando ya mwanagaza wa taa yake na kwa sababu amefanya kazi mchana kutwa anajiona vizuri juu ya kazi ambayo amefanya. (kif. 19) Hatufumi nguo zetu siku hizi bali ni saa nzuri ya kusuka sweta ikiwa uraishi katika nchi ya baridi na kutengeneza nguo ambazo zimeraruka.

Kila mwanamke anayo kazi ya kufanya na lazima atumie pesa ambazo anapewa kwa njia nzuri.

AGOSTI, 1967

MPANGO WA NNE

WAJIBI NA NGUO ZA MWANAMKE MKRISTO

Wimbo: Muda Mwingi Nilipotea' Uk. 71 'Nyimbo za Sifa'
Maandiko Natakatiifu: Mithali 31:21-31

Ombi

Wimbo: 'Sioshwi Dhambi Zangu' Uk. 90 'Nyimbo za Sifa'

Kutaja Majina

Shughuli

Mpango

Utangulizi: Twataka kujadilia leo juu ya wajibu wa Kikristo ambao tunao kwa jamaa zetu na majirani, na jinsi mwanamke Mkristo anavyovaa nguo zake ili afuate mwendo wa siku hizi kwa njia ya makini.

Sehemu ya I: (Vif. 21-22) Katika sehemu nyingi za ulimwengu kuna barafu na theluji na hali ya baridi kama ile tulionayo kwenye Mlima wa Kenya au Kilimanjaro. Huwa baridi katika miezi ya Julai na Agosti katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki lakini si baridi kama isemekanavyo katika kifungu hiki. Tunahitaji kuhakikisha kwamba tunazo nguo za joto na blanketi kabla ya Julai na Agosti kwa sababu tunafahamu kila mwaka tunatazamia kuwa na hali ya baridi katika sehemu za milima. Hatutaogopa hali ya baridi kwa jamaa zetu ikiwa tuko tayari.

Ikiwa hujui kushona unapaswa kuchukua nafasi ya kujifunza. Katika miji yetu mikuu kunazo senta kama Senta yetu ya Kibatisti katika Nairobi, Mombasa, na Dar es Salaam. Wanawake wetu katika Seminari ya Arusha wanafundishwa utunzaji wa nyumba. Tafuta mtu fulani katika jamii yako ambaye atakufundisha kutengeneza nguo na kushona. Ili ufanye hivi ununue nguo yako mwenyewe, sindano, uzi na mikasi. Kila mwanamke anapaswa kuwa na vitu hivi katika nyumba yake. Nunua sindano na uzi mwezi mmoja, mikasi katika mwezi mmoja, na nguo mwezi mwingine. Kumbuka kuwa